TANGAZO LA SERIKALI NA. 176 la tarehe 21/3/2025

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MRADI WA UENDELEZAJI NA UENDESHAJI WA KONGANI YA VIWANDA KWA KAMPUNI YA SINO TAN KIBAHA INDUSTRIAL PARK YA MWAKA 2025

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Mradi wa Uendelezaji na Uendeshaji wa Kongani ya Viwanda kwa Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park ya Mwaka 2025 na itaanza kutumika tarehe 26 Agosti, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa bidhaa zilizoainishwa katika Jedwali la Amri hii, zilizoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na au kwa niaba ya Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa bidhaa tajwa zitatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafika ukomo tarehe 26 Agosti, 2028 na inaweza kuongezwa kwa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park na Kituo cha Uwekezaji

Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| NA | BIDHAA | KIPIMO | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | Commuter Vehicle PSV- Coaster | NMB | 3 |

Dodoma,
11 Machi, 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*